

# Rasilimali za Wanaoshuhudia Tatizo

Kutokana na [ongezeko la vitendo vya chuki dhidi AAPI](#) wakati wa dharura ya COVID-19, ni muhimu kujua nini cha kufanya unaposhuhudia tatizo fulani. Ili kushughulikia suala hili, [Asian Americans Advancing Justice](#) na [Hollaback!](#) zimeandaa vikao vya mafunzo ya uingiliaji kati kwa wanaoshuhudia tatizo katika miezi ya Aprili na Mei. Ili kujiandikisha kwa kikao cha mafunzo, tembelea ukurasa wa [Mafunzo Pepe ya Uingiliaji Kati kwa Wanaoshuhudia Tatizo](#).

Hollaback! pia ina [Rasilimali za Uingiliaji Kati kwa Wanaoshuhudia Tatizo](#), zinazofundisha “5 Ds of Bystander Intervention.”

**KUVUTA MAWAZO (DISTRACTION)** ni njia hodari na bunifu ya kuingilia kati. Lengo hapa ni kuchelewesha tu tukio hilo kwa kulikatiza. Wazo ni kumpuuza mnyanyasaji na kumshirikisha moja kwa moja mtu anayelengwa. Usizungumzie au kurejelea unyanyasaji. Badala yake, zungumzia kuhusu jambo lisilohusiana kabisa. Unaweza kujaribu yafuatayo:

- Jifanye umepotea. Uliza ni saa ngapi. Jifanye unajua mtu anayenyanyaswa. [Zungumza nao kuhusu kitu chochote](#) na ukatize umakinifu kutoka kwa mnyanyasaji.
- Katiza maingiliano. [Endelea na ulichokuwa ukifanya](#), lakini katiza mwingiliano kati ya mnyanyasaji na mlengwa.
- Kwa makusudi mwaga kahawa yako, mwaga masalio kutoka kwa kipochi chako, au toa rabsha.

Kwa kweli, chunguza hali hiyo na uchague njia yako ya Kuvuta mawazo ipasavyo. Mtu anayelengwa ataelewa kinachoendelea baadaye, na pengine kitendo au mazungumzo yako yatakatiza hali hiyo.

**AGIZA (DELEGATION)** ni wakati unapomba usaidizi, rasilimali, au usaidizi kutoka kwa mtu mwingine. Hapa kuna mifano ya yale unayoweza kufanya:

- Pata msimamizi wa duka, dereva wa basi, au mfanyakazi wa usafirishaji na umwombe aingilie kati.
- Iwapo uko karibu na shule, wasiliana na mwalimu au mtu katika dawati la mapokezi. Kwenye eneo la chuo, wasiliana na usalama wa chuo au mtu katika dawati la mapokezi la jengo la chuo kikuu.
- Enda pamoja na rafiki yako na umwombe atumie mojawapo ya njia za Kuvuta Mawazo (kwa mfano kuuliza saa, maelekezo, au kuanzisha mazungumzo yasiyohusiana na unyanyasaji huo) ili kuwasiliana na mtu anayenyanyaswa wakati unapata mtu wa kuagiza usaidizi.
- Zungumza na mtu aliye karibu nawe ambaye ametambua kinachoendelea na anayeweza kuwa katika nafasi nzuri ya kuingilia kati. Shirikiana pamoja.
- Piga simu 311 au 911 (ikiwa ni salama kufanya hivyo) ili kuomba usaidizi. Kabla ya kuwasiliana na 911, tumia njia ya Kuvuta Mawazo ili kuwasiliana na mtu anayelengwa ili kuhakikisha kuwa

anataka ufanye hivi. Baadhi ya watu huenda wasipendeleo au wahisi kutokuwa salama kwa uingiliaji kati wa utekelezaji wa sheria. Kwa watu na jamii nyingi, historia ya kutendewa vibaya na utekelezaji wa sheria imesababisha hofu na kutokuaminiana na hatua za polisi, na kutokana na hali ilivyo sasa, kuna jamii nyingi, kama vile watu wasio na hati za kuwepo nchini, ambao wanaweza kuhisi kutokuwa salama mikononi mwa polisi. Katika hali fulani, huenda ukakosa kupata mtu katika hali hiyo, na unapojipata katika hali kama hiyo, utahitaji kutumia uamuzi wako bora.

Inaweza kusaidia sana kurekodi tukio kadri linavyotokea kwa mtu, lakini kuna mambo kadhaa ya kuzingatia ili **KUREKODI** unyanyasaji kwa usalama na uwajibikaji. Angalia [laha hii ya vidokezo](#) kutoka kwa SHAHIDI kwa maelezo zaidi.

Kwanza, tathmini hali hiyo. Je, kuna mtu yeyote anayemsaidia mtu anayenyanyaswa? Kama sivyo, tumia mojawapo wa D nne. Ikiwa mtu mwingine tayari anasaidia, tathmini usalama wako mwenyewe. Iwapo uko salama, endelea na uanze kurekodi. WAKATI WOTE muulize mtu aliyenyanyaswa kile angependa kufanya na rekodi. KAMWE usiichapishe mtandaoni au uitumie bila ruhusa yake. Kuna sababu kadhaa za hili. Kunyanyaswa au kuingiliwa kwa nguvu tayari ni hali inayofanya ujihisi mnyonge. Hatua ya kutumia picha au video ya mtu anayedhulumiwa bila idhini yake inaweza kumfanya mtu huyo ahisi kuwa mnyonge hata zaidi. Iwapo rekodi itatizamwa na watu wengi, inaweza kusababisha dhuluma zaidi na kiwango cha kujulikana ambacho mtu huyo hangependelea. Pia, kuchapisha video bila idhini ya mwathiriwa hufanya hali yake ijulikane kwa umma – jambo linaloweza kusababisha masuala mengi ya kisheria, hasa kama kitendo cha unyanyasaji au vurugu kilikuwa kinajumuisha baadhi ya makosa ya jinai. Anaweza kulazimika kujihusisha na mfumo wa sheria kwa njia ambayo hapendelei. Mwishowe, huenda hali hiyo ilisababisha kiwewe. Kuchapisha hali ya kiwewe ya mtu mwingine bila idhini yake sio njia fanisi na yenye manufaa kutoka kwa mtu anayeshuhudia tatizo.

Unaweza kutaka **KUKABILIANA MOJA KWA MOJA** na unyanyasaji kwa kutaja kile kinachoendelea au kumkabili mnyanyasaji. Mbinu hii inaweza kuwa hatari: mnyanyasaji anaweza kuelekeza unyanyasaji wake kwako na inaweza kuathiri hali hiyo vibaya zaidi. Kabla ya kuamua kukabiliana moja kwa moja, tathmini hali hiyo: Je, uko salama kimwili? Je, mtu anayenyanyaswa yuko salama kimwili? Je, inaonekana haiwezekani kwamba hali itakuwa mbaya zaidi? Je, unaweza kujua iwapo mtu anayenyanyaswa anataka mtu mwingine azungumzie hali hiyo? Iwapo unaweza kujibu ndiyo kwa maswali haya yote, unaweza kuchagua makabiliano ya moja kwa moja.

Iwapo unachagua kuingilia moja kwa moja, baadhi ya mambo unayoweza kumwambia mnyanyasaji ni:

- “Hilo halifai, linakosesha heshima, si sawa, nk.”
- “Achana naye.”
- “Huo ni ubaguzi dhidi ya wapenzi wa jinsia moja, ubaguzi wa rangi, (tumia aina ya unyanyasaji), nk.”

Jambo muhimu zaidi hapa ni kufanya tukio liwe fupi na wazi. Jaribu kutojihusisha na mazungumzo, mjadala, au malumbano, kwani hivi ndivyo hali huishia kuwa mbaya. Iwapo mnyanyasaji anajibu, jaribu kadiri uwezavyo kumsaidia mtu aliyelengwa badala ya kushirikisha mnyanyasaji.

Uingiliaji wa moja kwa moja unaweza kuwa hatari, kwa hivyo tumia njia hii kwa tahadhari.

Hata kama huwezi kuchukua hatua kwa wakati huo, unaweza kusaidia mtu aliyenyanyaswa kwa kumjulia hali baada ya kitendo. Aina nyingi za unyanyasaji hufanyika ukupita au kwa haraka sana, katika hali hiyo unaweza kusubiri hadi hali hiyo iishe na uzungumze na mtu aliyelengwa wakati huo. Hizi ni njia kadhaa za kutumia kikamilifu mbinu ya **KUCHELEWESHA (DELAY)**:

- Mwulize kama yuko sawa na umwaambie kuwa unasikitishwa na kilichotendelea.
- Mwulize kama kuna njia yoyote unayoweza kumsaidia.
- Jitolee kuongozana naye kwenda mahali anakoenda au kuketi chini pamoja naye kwa muda mfupi.
- Shiriki rasilimali naye na ujitolee kumsaidia ili kuandikisha ripoti ikiwa anataka.
- Kama umerekodi tukio hilo, mwulize kama angependa umtumie.

**\* Kidokezo kuhusu usalama:** Hatungependa upate madhara ukijaribu kumsaidia mtu mwingine. Wakati wote fikiria kuhusu usalama na uzingatie hali ambazo haziwezi kumweka mtu mwingine katika madhara.